TANGAZO LA SERIKALI NA. 694 la tarehe 02/12/ 2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MATANDALANI YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Matandalani ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P 1 iliyopo karibu na mto Mtisi yenye majira - nukta 293687.237E, 9278973N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S 04º 54' 37" W hadi alama ya mpaka ya upimaji namba P 2 yenye majira - nukta 293396.241E, 9275586.805N; kwa umbali wa kilomita 3.399, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S 88º 16' 18" E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 830 yenye majira - nukta 296770.000E, 9275485.000N; kwa umbali wa kilomita 3.375, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi kwa uelekeo wa S 62º 19' 17" W hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 652 yenye majira - nukta 292450.000E, 9273219.000N kwa umbali wa kilomita 4.878 ukikatiza barabara ya Mpanda / Sumbawanga; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N 63º 40' 06" W hadi alama ya mpaka ya upimaji namba

*Tangazo la Serikali na. 694 (linaendelea)*

WL 693 yenye majira - nukta 288417.000E, 9275215.000N kwa umbali wa kilomita 4.499; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa N 34$^{o}$ 02’ 32” E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 692 yenye majira - nukta 290337.000E, 9278057.000N kwa umbali wa kilomita 3.429; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kwa uelekeo wa N 18$^{o}$ 22’ 05” E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 663 yenye majira - nukta 290763.000E, 9279340.000N karibu na mto Magula na barabara ya Sumbawanga / Mpanda kwa umbali wa kilomita 1.351; baada ya hapo mpaka unakatiza barabara Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S 82$^{o}$ 51’ 55” E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba P I yenye majira ya nukta 293687.237 ulipoanzia.”

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*